**Disclaimer : Ministry of Finance and Planning repository shall be regarded as a publisher and bears no liability for any damage upon using contents of the repository.**

MoF Journals

MoF Journals

2024

# Hazina Yetu

United Republic, Tanzania

https://repository.mof.go.tz/handle/123456789/801

*Downloaded from Ministry of Finance and Planning Repository*

# HAZINA YETU

## TOLEO LA KWANZA MWAKA 2024/25

JARIDA LA HAZINA YETU - TOLEO LA KWANZA MWAKA 2024/2025

JARIDA LA HAZINA YETU - TOLEO LA KWANZA MWAKA 2024/2025

JARIDA LA HAZINA YETU - TOLEO LA KWANZA MWAKA 2024/2025












# Kutoka Dawati la Mhariri Mkuu



Karibu ujisomee Jarida la Hazina Yetu la Wizara ya Fedha, liliko katika mfumo wa nakala laini na nakala ngumu, linaloandaliwa na na kuzalishwa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini, Wizara ya Fedha.

Jarida hili linatolewa kila Robo Mwaka ikiwa ni utekelezaji wa Mkakati wa Mawasiliano wa Wizara, wenye lengo la kuwahabarisha wadau wetu namna Wizara inavyotekeleza majukumu yake ikiwemo usimamizi wa Sera za Fedha na Uchumi, Programu, Matukio na Mikakati mingine ya kusimamia uchumi wa nchi.

Miongoni mwa habari na matukio tuliyokuandalia katika Jarida hili ni pamoja na Sheria Mpya ya Ununuzi, Maendeleo ya Sekta ya Uhasibu nchini, Historia ya Wizara ya Fedha pamoja na habari za matukio mbalimbali liliyojiri katika kipindi cha Robo ya Kwanza ya Mwaka wa Fedha 2024/2025 (Julai hadi Septemba, 2024).

Ninakutakia usomaji mwema.

Asante sana

**Benny Mwaipaja**

**Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**



# MAKALA

# IFAHAMU WIZARA YA FEDHA

*Na. Eva Valerian Ngowi*

WIZARA ya Fedha ni moja kati ya Wizara zilizoanzishwa baada ya uhuru wa Tanganyika mwaka 1961 na kuanza kutekeleza majukumu yake mwaka 1962 baada ya Hati ya majukumu kutolewa na Serikali na kuainisha wajibu wa kila Wizara.

Kufuatia mabadiliko mbalimbali ya uongozi wa nchi, Wizara ya Fedha nayo ilipitia mabadiliko hayo kwa lengo la kuongeza ufanisi katika usimamiaji wa shughuli za Serikali.

Mabadiliko hayo yalilenga katika maeneo ya uongozi na majukumu na kusababisha jina la Wizara kubadilika mara kwa mara kwa lengo la kukidhi utekelezaji wa majukumu iliyopangiwa ambapo mwaka 1962 ilijulikana kama Wizara ya Fedha.

Mwaka 1967 ilibadilishwa kuwa Wizara ya Fedha na Mipango, mwaka 1983 iliitwa Wizara ya Nchi, Mipango na Uchumi; mwaka 2008 ilikuwa Wizara ya Fedha na Uchumi, mwaka 2010 ilirudi kuwa Wizara ya Fedha, mwaka 2015 ilikuwa Wizara ya Fedha na Mipango na Julai 2023 Serikali ilibadilisha jina kuwa Wizara ya Fedha.

Wizara ya Fedha ina jukumu la kusimamia mapato, matumizi na fedha za Serikali na kutoa ushauri kwa Serikali kuhusu masuala ya fedha na uchumi.

Vilevile, Wizara ina mamlaka ya kusimamia uundaji wa Sera za Kodi, udhibiti wa fedha, mapato, benki, bima, uhasibu, manunuzi ya umma, sera za mikopo na usimamizi wa mikopo, kuratibu fedha na misaada kutoka kwa washirika wa maendeleo.,

Wizara ya Fedha iliongozwa na Mawaziri mbalimbali akiwemo Sir. Ernest Vassey kuanzia mwaka 1960 hadi 1961, Mhe. Paul M. Bomani kuanzia mwaka 1962 hadi 1965; Mhe. Amir H. Jamal kuanzia mwaka 1966 hadi 1972, Mhe. Cleopa D. Msuya kuanzia mwaka 1973 hadi 1975, Mhe. Edwin Mtei kuanzia mwaka 1978 hadi 1981.

Aidha, Mhe. Prof. Kighoma A. Malima aliongoza Wizara kuanzia mwaka 1983 hadi 1985 na mwaka 1993 hadi 1994, Mhe. Stephene A. Kibona kuanzia mwaka 1990 hadi 1993, Mhe. Jakaya M. Kikwete kuanzia mwaka 1994 hadi 1995, Mhe. Prof. Simon M. Mbilinyi kuanzia mwaka 1995 hadi 1996, Mhe. Daniel N. Yona kuanzia mwaka 1997 hadi 2000, na Mhe. Basil P. Mramba kuanzia mwaka 2001 hadi 2005.

Mawaziri wengine ni Mhe. Zakhia H. Meghji kuanzia mwaka 2005 hadi 2007, Mhe. Mustapha H. Mkulo kuanzia mwaka 2008 hadi 2012, Mhe. Dkt. Willium A. Mgimwa kuanzia mwaka 2012 hadi 2014, Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum kuanzia mwaka 2014 hadi 2015, Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango kuanzia mwaka 2015 hadi 2021 na kuanzia mwaka 2021 hadi sasa ni Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Madelu.


MHE. SIR. ERNEST VASSEY
1962 -1965


MHE. PAUL M. BOMANI
1962 -1965


MHE. AMIR H. JAMAL
1966-1972; 1976 -1977; 1982


MHE. CLEOPA MSUYA
1973-1975; 1986 -1989


MHE. EDWIN MTEI
1978-1981


MHE. PROF. KIGHOMA A. MALIMA
1983 -1985; 1993 - 1994


MHE. STEPHEN A. KIBONA
1990 -1993


MHE. JAKAYA MRISHO KIKWETE
1994 - 1995


MHE. PROF. SIMON MBILINYI
1995 - 1996


MHE. DANIEL YONA
1997- 2000


MHE. BASIL P. MRAMBA
2001 - 2005


MHE. ZAKHIA H. MEGHJI
2005 - 2007


MHE. MUSTAPHA H. MKULO
2008 - 2012


MHE. DKT. WILLIAM A. MGIMWA
2012 - 2014


MHE. SAADA MKUYA SALUM
2014 - 2015


MHE. DKT. PHILIP I. MPANGO
2015 - 2021


MHE. DKT. MWIGULU L. NCHEMBA
2021-SASA




Kwa sasa kutokana na muundo ulioidhinishwa na mgawanyo wa majukumu, Wizara ya Fedha ina Idara 13 na Vitengo sita (6) ambavyo ni Idara ya Uchambuzi wa Sera, Idara ya Usimamizi wa Madeni, Idara ya Uendelezaji Sekta ya Fedha, Idara ya Fedha za Nje, Idara ya Usimamizi wa Bajeti ya Serikali, Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali na Idara ya Mkaguzi wa Ndani Mkuu.

Idara nyingine ni Idara ya Usimamizi wa Mifumo ya Fedha na Tehama, Idara ya Usimamizi wa Mali za Serikali, Idara ya Sera za Manunuzi, Idara ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu, Idara ya Mipango na Idara ya Huduma za Sheria.

Vitengo vya Wizara ni Kitengo cha Mawasiliano Serikalini, Kitengo cha Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, Kitengo cha Ufuatiliaji na Tathmini, Kitengo cha Uhasibu (Fungu 50, 21, 23, 01, 22 na 06), Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani (Fungu 50, 21, 23, 01, 22 na 06) na Kitengo cha Usimamizi wa Ununuzi.

Majukumu ya Wizara yanatekelezwa kupitia Idara na Vitengo vyake ambayo yataelezwa kwa kina kupitia Makala zijazo.


# KADA YA UHASIBU CHACHU YA MAENDELEO AFRIKA

*Na. Peter Haule*

Tanzania ni miongoni mwa nchi barani Afrika ambayo inatumia Kada ya Uhasibu katika shughuli zake za maendeleo kwa kuwa malipo ya Serikali yanayokwenda kwenye miradi ya maendeleo hupitia mchakato wa Wataalam wa Kada hii.

Katika kuimarisha kada hii, Nchi za Afrika zilianzisha Umoja wa Wahasibu Wakuu wa Serikali wa Nchi za Afrika (African Association of Accountants General (AAAG), Tanzania ikiwa ni miongoni mwa nchi mwanzilishi wa Umoja huo, ambapo madhumuni yake ni kuhakikisha hakuna nchi itakayobaki nyuma katika kutumia Kada hii kuleta maendeleo ya nchi wanachama.

Umoja wa Wahasibu Wakuu wa Serikali Afrika pia umekuwa ukifanya Mkutano wake Mkuu kila mwaka (African Association of Accountants General (AAAG), ambapo mwaka huu, Tanzania imebahatika kuwa Mwenyeji wake, ukiwa ni Mkutano wa Piili kufanyika tangu kuanzishwa kwake, na utafanyika katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano-Arusha (AICC), kwa muda wa Siku Nne jijini Arusha, kuanzia tarehe 2 hadi 5 Disemba, 2024, ukiwa na lengo la kuimarisha utendaji kazi wa Kada hiyo.



Kujenga imani ya umma katika Mifumo ya Usimamizi wa Fedha za Umma kwa Ukuaji Endelevu (Building Public Trust in PFM Systems for Sustainable Growth).

Akizungumza wakati wa maandalizi ya Mkutano huo, jijini Arusha, Mhasibu Mkuu wa Serikali, CPA Leonard Mkude alisema katika kuhakikisha Wahasibu wanatekeleza majukumu yao ya kulipatia Bara la Afrika maendeleo ni lazima kuwa na maazimio ya pamoja kupitia Chombo kinachowaweka katika mwamvuli mmoja.

Alisema Mkutano huo unatarajiwa kuwa na washiriki zaidi ya 2,000 unawakutanisha Wahasibu, Wakaguzi wa Hesabu, Wataalamu wa masuala ya Fedha, Tehama, Wataalamu wa Vihatarishi, wakiwemo walioajiriwa Serikalini, Kampuni binafsi pamoja na waliojiajiri.

CPA Mkude alisema kuwa , faida za Mkutano huo ni pamoja na kuwa na Afrika yenye mafanikio yenye msingi wa ukuaji jumuishi na maendeleo endelevu, Bara jumuishi lililounganishwa kisiasa na kwa kuzingatia maadili ya Pan-Africanism na maono ya mwamko wa Afrika na kuwa na Afrika yenye utawala bora, demokrasia, kuheshimu haki za binadamu na utawala wa sheria, kuwa na Afrika yenye amani na usalama, utambulisho thabiti wa kitamaduni, urithi wa pamoja na maadili.

Alieleza kuwa kutokana na umuhimu wa Kada ya Uhasibu, Mkutano wa AAAG, ulitarajiwa kufunguliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.


Kwa upande wake Mwenyekiti wa Umoja wa Wahasibu wa Afrika, ambaye pia ni Mhasibu Mkuu kutoka Lesotho, Bi. Malehlohonolo Mahase, alisema Mkutano wa Wahasibu Afrika unafanyika Tanzania kwa kuwa ni mwanachama anayeaminika na amekuwa mshiriki mwaminifu katika Umoja huo na kwamba wajumbe wa Mkutano huo watajifunza namna Tanzania ilivyopiga hatua kubwa katika matumizi na usimamizi wa Mifumo ya Fedha.



Alisema kuwa Tanzania imepiga hatua kubwa katika kutekeleza na kusimamia viwango vya kimataifa vya kihasibu, imekuwa ya mfano katika ukuaji wa uchumi, imeimarika katika suala la ukarimu wa wageni, maendeleo katika Teknolojia ya Habari na Mawasiliano na ni miongoni mwa nchi zenye vivutio vingi vya utalii, hivyo wanachama watakaohudhuria Mkutano huo watapata fursa ya kushuhudia mafanikio hayo.

Mkutano huu utatoa fursa ya kuya kutanisha makundi mbalimbali wakiwemo ya wafanyabiashara wakubwa, wa kati na wadogo kutoka Barani Afrika na utawasaidia katika kukuza biashara zao kwa kuwajengea uwezo katika masuala ya fedha ikiwemo namna ya kuripoti hali ya uchumi Barani Afrika, jambo ambalo litaongeza uwazi na uwajibikaji katika usimamizi wa fedha.



# SHERIA MPYA YA UNUNUZI KUONGEZA UWAZI NA TIJA

*Na Josephine Majura*

Itakumbukwa kuwa Septemba 7 mwaka 2024, Serikali iliwasilisha bungeni, Muswada wa Sheria ya Ununuzi wa Umma wa mwaka 2023, huku ikiainisha faida nane zitakazotokana na Sheria hiyo. Miongoni mwa faida hizo ni kuimarisha mazingira ya ununuzi na ugavi kwa taasisi na mashirika ya umma yanayojiendesha kibiashara.

Akiwasilisha muswada huo bungeni, Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), alisema lengo la kutungwa kwa Sheria hiyo ni kuweka masharti bora ya usimamizi wa ununuzi wa umma, ugavi na uondoshaji wa mali kwa njia ya zabuni.



*Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), akiwasilisha bungeni muswada wa Sheria ya Ununuzi wa Umma wa mwaka 2023.*

Ili Sheria hiyo ya Manunuzi Sura na. 410 iweze kutekelezwa kikamilifu, Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na wadau wa sekta ya Ununuzi wa umma, imeanza kutoa mafunzo kwa watalaamu wa ununuzi wa umma nchini, ili kwenda sambamba na mabadiliko yaliyoainishwa katika Sheria hiyo.

Mafunzo hayo yaliyotolewa na Wizara kupitia Taasisi zake ambazo ni Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA), Kituo cha Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPPC) na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), yanalenga kuwajengea uwezo Wakuu wa Idara ya Ununuzi na Mipango nchi nzima.

Kwa kuanza, mafunzo hayo yalitolewa katika ngazi ya Kanda ambazo ni Kanda ya Ziwa, Kanda ya Kati, Kanda ya Pwani, Kanda ya Kaskazini, Kanda ya Kusini, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na Kanda ya Magharibi.

Sheria hiyo itaimarisha usimamizi wa mikataba ya ununuzi, kuongeza ufanisi katika mnyororo wa ugavi na kupunguza muda katika hatua na michakato ya zabuni, hii ni kutokana na matumizi ya mfumo wa ununuzi na ugavi kwa njia

ya kielektroniki (NeST) na uondoshwaji wa mali za Serikali kwa njia ya zabuni.

Sheria hiyo imeweka masharti ya bei kikomo kwa baadhi ya bidhaa na huduma katika ununuzi wa umma na hivyo kudhibiti gharama na kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa miradi kwa utaratibu wa *force account.*

Sheria hii imekuja wakati muafaka kwa sababu imetungwa kudhibiti urasimu katika uidhinishaji wa zabuni hivyo kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa shughuli za mnyororo wa ugavi.

Kumekuwa na janga kubwa la uadilifu katika tasnia ya ununuzi wa umma, hivyo Sheria hii imekuja na mwarobaini kwa kuweka sharti la kudhibiti viwango vya weledi na uzoefu wa watekelezaji wa miradi ya ujenzi, kwa utaratibu wa force account na kutokuweka viwango vya ukomo wa uidhinishaji wa zabuni.

Baada ya Matumizi ya Sheria hii, makundi mbalimbali yamefaidika kutokana na kufanya kazi za Serikali kupitia mfumo wa ununuzi wa kieletroniki, ambapo kuanzia Julai 1, 2024 hadi sasa, makundi maalum yapatayo 26 yalipata zabuni za Serikali zenye thamani ya zaidi ya shilingi milioni 900. Makundi hayo yanahusisha vijana, wazee, wanawake na watu wenye mahitaji maalum.

Aidha, Sheria mpya ya Ununuzi imeweka upendeleo kwa makundi maalum, ambapo Taasisi nunuzi zinapaswa kutenga asilimia 30 ya Mpango wa Ununuzi wa mwaka kwa ajili ya vijana, wanawake, wazee na watu wenye mahitaji maalum.

Makundi haya yatanufaika na zabuni zenye thamani ya hadi shilingi milioni 500 kwa zabuni moja kwenye bidhaa, huduma na kazi za ujenzi.

Kwa mujibu wa Sheria hii, ni kosa la jinai kwa Taasisi Nunuzi kutotekeleza masharti ya takwa hili la kisheria, na Taasisi itakayoshindwa kutekeleza masharti hayo kutokana na sababu zozote zile inapaswa kutoa Taarifa kwenye Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA).

Sheria inatoa fursa kwa kampuni za ndani kuingia ubia na kampuni za nje ambapo kampuni za ndani zitakuwa kiongozi wa ubia huo.

Pia Sheria hii imeweka sharti la upendeleo kwa bidhaa zilizotengenezwa, kuchimbwa au kuzalishwa nchini hadi wa asimilia 15 na sharti la Taasisi nunuzi kununua bidhaa, huduma na kazi za ujenzi kwa kuzingatia bei ya kikomo.

Sheria hii pia imeweka adhabu ya kinidhamu kwa mtumishi atakayenunua bidhaa, huduma au kazi za ujenzi kwa bei ya juu kuliko bei ya kikomo na kuweka utaratibu wa ununuzi kwa taasisi za umma zinazojiendesha kibiashara.

Sheria imeweka masharti ya utaratibu wa ununuzi kwa taasisi hizo zinazojiendesha kibiashara, na kanuni imeruhusu tamko la dhamana badala ya dhamana ya kibenki kwa zabuni zenye thamani hadi ya sh. bilioni 50.

Aidha, Sheria hii imeweka ukomo maalum wa uidhinishaji kwa Afisa Masuuli ili kupunguza mchakato wa ununuzi na kuidhinisha mpaka wastani wa shilingi bilioni 10 bila kuhitaji bodi ya zabuni kwa bidhaa, huduma na kazi za ujenzi na kuweka utaratibu na ukomo wa matumizi ya nyongeza kwenye matumizi ya rasilimali za ndani *'Force Account'.*

Sheria imeweka sharti la lazima la matumizi ya mfumo ambapo hadi kufikia Septemba mwaka 2024, Taasisi zipatazo 30,315, wazabuni 25,108 na vikundi 425 vimesajiliwa na kupewa mikataba ya ununuzi yenye thamani ya shilingi bilioni 2.8.



# MIRADI YA MAENDELEO MWANZA KUCHOCHEA UCHUMI

*Na Asia Singano*

Serikali ya Awamu ya Sita imeleta mageuzi makubwa ya miundombinu yenye lengo la kuchochea maendeleo katika nyanja za kijamii na kiuchumi ambayo inasadifu matumizi mazuri ya fedha za umma kwa maendeleo ya nchi..

Akikagua miradi ya maendeleo katika Mkoa wa Mwanza, Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt.Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), alisema kuwa Serikali imeendelea kutoa fedha nyingi wakati huu kuliko wakati wowote ule ambapo kila mahali nchini inatekelezwa miradi ya maendeleo ikiwemo Reli-SGR, Umeme wa Bwawa la Julius Nyerere, Ujenzi wa Daraja la Kigongo-Busisi na mingine mingi katika Sekta za uzalishaji, afya, maji na elimu.

Mhe. Dkt. Nchemba alimhakikishia mwenyeji wake, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Mhe. Said Mohamed Mtanda, kuwa Serikali itahakikisha kuwa miradi yote ya kimkakati na mingine inayogusa maisha ya wananchi mkoani humo, inaendelea kupatiwa fedha ili kusisimua uchumi wa nchi pamoja na



kuboresha maisha ya wananchi.

Aidha, wakati wa ukaguzi wa ujenzi wa mradi wa Soko Kuu la Mwanza, Dkt. Nchemba alieleza kuwa mradi huo utasaidia kuongeza mapato ya Halmashauri ya Jiji la Mwanza, ambapo jumla ya shilingi bilioni 3.5 zinatarajiwa kukusanywa kwa mwaka na kwamba mpaka sasa mradi huo umetoa ajira kwa vijana wapatao 175 ambao walikuwa wakiendelea na kazi mbalimbali za ujenzi.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Mhe. Saidi Mohamed Mtanda, alimpongeza Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kutoa fedha nyingi zinazotumika kutekeleza miradi ya maendeleo ya wananchi ikiwemo miradi mikubwa ya kimkakati.

Mhe. Mtanda alisema hayo wakati wa ukaguzi wa ujenzi wa soko Kuu la Mwanza na kueleza kuwa mradi wa ujenzi wa Soko



Kuu la Mwanza, Mjini Kati, umegharimu kiasi cha shilingi bilioni 23.4, na ni Mradi ambao utakapokamilika, utawezesha wafanyabiashara wapatao 1,400 kupata maeneo mazuri ya kufanyia biashara.

Mradi huo utakuwa na maduka 514, vizimba 332 vya matunda na mbogamboga, vizimba 372 vya nafaka, mama lishe maeneo 12, eneo kwa ajili ya wafanyabiashara ndogondogo (Machinga 167), ofisi 5, eneo moja la kukusanyia takataka, eneo la maegesho ya magari madogo 192 chini ya usawa wa ardhi (basement) na vyoo.

Mhe. Dkt Nchemba alitembelea na kukagua ujenzi wa majengo ya Taasisi ua Uhasibu Tanzania (TIA) Tawi la Mwanza ambapo, akitoa taarifa ya maendeleo ya ujenzi wa mradi wa Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA), Afisa Mtendaji Mkuu wa Taasisi hiyo, Prof. Wiliam Pallangyo, alimweleza Mhe. Nchemba kuwa TIA imepatiwa Jumla ya shilingi bilioni 85.7 kwa ajili ya ujenzi wa mabweni na miundombinu ya kufundishia na kujifunzia, ambapo shilingi bilioni 58.1 ilitolewa na Serikali ya awamu ya sita kwa ajili ya kuhudumia kampasi za Mtwara(bilioni 6.1), Mbeya (bilioni 3.2), Mwanza (bilioni 7.8), Kigoma (bilioni 11) na Zanzibar shilingi (bilioni 30), na shilingi bilioni 27.6 iliyotolewa kupitia mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET), kwa ajili ya ujenzi wa kampasi ya Mwanza na Singida.

Prof. Pallangyo TIA aliongeza kuwa kampasi ya Mwanza, , alieleza kuwa ilianzishwa mwaka 2012 ikilenga kusogeza huduma karibu zaidi na wakazi wa mikoa ya Kanda ya Ziwa. ambapo awali Kampasi hiyo ilitumia majengo ya kukodi eneo la Buzuruga, Kata ya Nyakato-Manispaa ya Ilemela.

Profesa Pallangyo, Alisema kuwa Kampasi hiyo iliongeza idadi ya wanafunzi kutoka 305 mwaka 2012/2013 hadi kufikia wanafunzi 1,792, mwaka 2023/2024. Ukuaji huo unatokana na ongezeko la shule za msingi na sekondari, sambamba na mpango wa elimu bila malipo.



Ujenzi wa Kampasi ya Mwanza, unajumuisha madarasa yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,980 kwa wakati mmoja, maabara ya kisasa ya kompyuta yenye uwezo wa kuhudumia wanachuo 200 kwa wakati mmoja, maktaba yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 250 kwa wakati mmoja na vyumba vya ofisi 10.

Kwa ujumla majengo hayo yana uwezo wa kuhudumia kwa wakati mmoja watu 2,430 kwa sasa mradi umekamilika kwa asilimia 99 na unatarajiwa kuzinduliwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Serikali ya Awamu ya sita imekuwa na utaratibu wa kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo ili kuhakikisha pesa zinazoelekezwa katika utekelezaji wa miradi hiyo zinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa na kuwaletea wananchi maendeleo.





**Usikae Gizani!! Lipia Sasa Luku kupitia GePG App popote ulipo!!**

Unaweza pia kutumia U.S.S.D Code ***152*00#** au kwa kutumia Menu za Mitandao ya Simu.

**Pakua sasa kupitia App Store na Play Store**



# MATUKIO YALIYOJIRI



# DKT. NCHEMBA AONGOZA MAWAZIRI WENZAKE KATIKA KIKAO NA MAKAMU WA RAIS WA BENKI YA DUNIA

*Na. Joseph Mahumi*

Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), amewaongoza Mawaziri wenzake; Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Angellah Kairuki (Mb) na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mhe. Jerry Silaa (Mb), katika kikao na Makamu wa Rais wa Benki ya Dunia, anayesimamia nchi za Kanda ya Mashariki na Kusini mwa Afrika, Bi. Victoria Kwakwa, aliyefika nchini katika ziara ya kikazi, ambapo katika kikao hicho, Serikali na Benki ya Dunia, walijadiliana masuala ya msingi ya kuendeleza ushirikiano kati ya pande hizo mbili ikiwemo uhifadhi na utalii pamoja na maendeleo ya watu na Taifa kwa ujumla.

Akizungumza kwa niaba ya Serikali, Mhe. Dkt. Nchemba aliishukuru Benki ya Dunia kwa mchango wake mkubwa katika maendeleo ya Taifa kupitia ufadhili wa program na miradi mbalimbali inayotekelezwa hapa nchini kwa manufaa ya wananchi wake.

Alimweleza Kiongozi huyo kwamba katika Mwaka wa fedha wa 2024, uchumi wa Tanzania unatarajiwa kukua kwa asilimia 5.4 na utaongezeka kukua kwa asilimia 6.0 katika muda wa kati katika kipindi cha mwaka 2025/2027, hatua inayochangiwa na maboresho ya sera mbalimbali zinazo



boresha mazingira ya uwekezaji na ufanyaji biashara na uwekezaji katika sekta muhimu za uzalishaji.

Bi. Kwakwa alisifu na kupongeza ushirikiano uliopo kati ya Tanzania na Benki hiyo na kwamba Tanzania imekuwa nchi inayofanya vizuri kiuchumi kati ya nchi nyingi za Kusini mwa Jangwa la Sahara na ni mnufaika mkubwa wa programu mbalimbali zinazoendeshwa na Taasisi hiyo kubwa ya Fedha Duniani.

Makamu wa Rais wa Benki ya Dunia Bi. Victoria Kwaka, alikuwa nchini kwa ziara ya kikazi ya siku mbili ambapo alikutana na kufanya mazungumzo na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ikulu Jijini Dar es Salaam.









# TANZANIA NA DENMARK KUIMARISHA ZAIDI USHIRIKIANO WA KIUCHUMI

*Na Benny Mwaipaja*

Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), ameihakikishia Denmark kwamba Tanzania iko tayari kushirikiana na nchi hiyo kupitia Mkakati wake Mpya wa Ushirikiano wa Kimataifa kwa kuishirikisha sekta binafsi katika mipango yake ya maendeleo ili kukuza uchumi na ajira.

Dkt. Nchemba aliyasema hayo alipokutana na kufanya mazungumzo na Waziri wa Ushirikiano wa Maendeleo na Sera za Mabadiliko ya Tabianchi wa Denmark, Mhe. Dan Jørgesen, jijini Dodoma.

Dkt. Nchemba, alisema kuwa Tanzania ina fursa kubwa za uwekezaji katika sekta mbalimbali na kutoa wito kwa kampuni, mashirika na taasisi mbalimbali kutoka Denmark, kushirikiana na sekta binafsi ya Tanzania kuwekeza mitaji na teknolojia ili pande zote mbili ziweze kunufaika.

Alisema kuwa mkazo mkubwa wa Serikali ya Awamu ya Sita, inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, ni kuhakikisha Sekta binafsi inaendesha uchumi wa nchi na kwamba ili kufanikisha mpango huo, Serikali imefanya mageuzi makubwa ya kisera na kisheria ili kuboresha mazingira ya uwekezaji nchini.



Dkt. Nchemba aliyataja baadhi ya maeneo yanayohitaji ushiriki wa sekta binafsi kuwa ni pamoja na uendeshaji wa reli ya kisasa ya SGR, nishati, kilimo, na maeneo mengine kadha wa kadha.

Alisema kuwa Tanzania iko tayari kushirikiana na Denmark kupitia mpango wake mpya wa ushirikiano baada ya kusitisha uamuzi wake wa wa kufunga Ofisi za Ubalozi wake nchini, ambapo nchi hiyo imepanga kuongeza kiwango cha ufadhili na kuelekeza fedha hizo kwenye maeneo yatakayokuza uchumi, ikiwemo nishati, kuboresha mifumo ya kodi, kilimo, elimu, afya, pamoja na kusaidia sekta binafsi.

Dkt. Nchemba aliishukuru Denmark kwa kuendeleza ushirikiano wake uliotimiza miaka 60, ambapo katika miaka ya hivi karibuni, nchi hizo mbili zilikuwa zikitekeleza miradi ambayo Denmark iliipatia Tanzania msaada wa takriban Denish Krone bilioni 2, sawa na shilingi za Tanzania, bilioni 646.

Aidha, alisema kuwa Denmark kupitia Shirika lake la Maendeleo (DANIDA), imetoa zaidi ya shilingi bilioni 103 zinazotokana na mapato ya uwekezaji wake wa hisa katika Benki ya CRDB, ambazo zimetumika kwa ajili ya kusaidia sekta ya afya kupitia Mfuko wa Afya.

Aliiomba pia Denmark kupitia Taasisi yake inayohusika na masuala ya Bima na Dhamana (Danish Export Credit Agency), kushiriki katika ujenzi wa mradi wa SGR kwa vipande vilivyobaki kutokana na umuhimu wa mradi huo katika kukuza biashara na ustawi wa maisha ya watu watakaotumia reli hiyo pamoja na kukuza pato la Taifa.

Kwa upande wake, Waziri wa Ushirikiano wa Maendeleo na Sera za Mabadiliko ya Tabianchi wa Denmark, Mhe. Dan Jørgesen, alimpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa hatua kubwa ambayo nchi imepiga kiuchumi licha ya ulimwengu kukabiliwa na changamoto mbalimbali na kwamba anaiona Tanzania kuwa moja ya nchi kubwa kiuchumi kwa siku zijazo.

Aliishauri Tanzania, kuishauri Denmark namna ya kuboresha ushirikiano na maeneo ya kimkakati ambayo nchi inataka kuyapa kipaumbele hususan katika eneo la uwekezaji na biashara.

katika Mpango wake Mpya wa Ushirikiano na Nchi za Afrika, ambao nchi yake inauandaa na wanatarajia utazinduliwa na Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambaye amealikwa kuitembelea nchi hiyo.

Mkutano huo ulihudhuriwa pia na Naibu Waziri wa Maendeleo wa Serikali ya Denmark, Mhe. Lotte Machon, Balozi wa Denmark nchini Tanzania, Mhe. Mette Dissing-Spandet, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Dkt. Natu El-maamry Mwamba, Balozi wa Tanzania katika nchi za Scandinavia, Mhe. Dkt. Grace Olotu, na Balozi wa Tanzania wa Heshima nchini Denmark, Mhe. Simon Mears na Viongozi wengine waandamizi wa Wizara ya Fedha, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Serikali ya Denmark.



# WATANZANIA ASILIMIA 80 KUFIKIWA NA ELIMU YA FEDHA



*Na. Saidina Msangi*

Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na wadau na Taasisi zilizo chini yake imejipanga kutoa elimu ya fedha kwa Watanzania asilimia 80 ifikapo mwaka 2025 ili kuwawezesha wananchi kufahamu umuhimu wa akiba, bima, usimamizi wa fedha binafsi pamoja na kutumia watoa huduma rasmi wa fedha waliosajiliwa.

Hayo yalibainishwa na Afisa Usimamizi wa Fedha kutoka Wizara ya Fedha, Bw. Stanley Kibakaya, wakati wa kuhitimisha programu ya utoaji wa elimu ya fedha kwa wananchi katika ukumbi wa mikutano wa Ofisi ya Halmashauri ya Mji Kibaha, mkoani Pwani.

Alisema kuwa elimu hiyo ya fedha imepokelewa vizuri na wananchi katika mikoa ya Kagera, Manyara, Singida, Kigoma, Rukwa, Simiyu, Shinyanga, Tabora, Mtwara, Morogoro, Lindi na alibainisha kuwa mikoa mingine inatarajiwa kufikiwa katika awamu zijayo.

*"Tunafanyia kazi maelekezo ya Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa Wizara ya Fedha kuendelea kutoa elimu ya fedha kwa wananchi ili kuwawezesha kuondokana na mikopo umiza,''alisema Bw. Kibakaya.*



Alisema kuwa kumekuwa na muitikio mkubwa wa kuhudhuria katika programu za elimu ya fedha na wananchi wamefurahishwa na kukiri kuwa elimu hiyo imewasaidia na wataenda kuzitumia huduma rasmi za fedha ikiwemo kuweka akiba, uwekezaji na bima.



Kwa upande wao baadhi ya wananchi wa Mji wa Kibaha, mkoani Pwani, walioshiriki mafunzo hayo waliipongeza Serikali kwa kuwapatia elimu hiyo muhimu ambayo walieleza kuwa itawawezesha kujikwamua kiuchumi pamoja na kujiandaa kutumia fursa za uwekezaji katika mifumo rasmi.







# JAPAN YAONGEZA SH. BILIONI 8.9 UKARABATI WA BANDARI YA KIGOMA

*Na. Scola Malinga na Peter Haule,*

Tanzania imepokea msaada wa nyongeza wa Yen za Japan milioni 548 sawa na shilingi bilioni 8.9 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa ukarabati wa Bandari ya Kigoma baada ya marekebisho ya mikataba miwili ya msaada kati ya Tanzania, Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Japan (JICA) na Ubalozi wa Japan.

Mikataba ya marekebisho ya msaada ilisainiwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Dkt. Natu El-maamry Mwamba kwa niaba ya Serikali ya Tanzania, Balozi wa Japan nchini Tanzania, Mhe. Yasushi Misawa na Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Japan Tanzania, Bw. Hitoshi Ara, kwa niaba ya Japan.

Akizungumza baada ya kusainiwa kwa marekebisho ya mikataba hiyo, Dkt. Mwamba alisema kuwa awali, Serikali ya Japan kupitia mikataba iliyosainiwa Februari 4, 2022 ilitoa msaada wa Yen za Japan bilioni 2.73 sawa na shilingi bilioni 44.42 kwa ajili ya ukarabati wa Bandari hiyo.

*Jumla ya msaada uliotolewa na Serikali ya Japan unakuwa Yen za Japan bilioni 3.27 sawa na shilingi bilioni 53.35, ambapo fedha zilizoongezwa zinalenga kuziba pengo lililotokana na kuporomoka kwa thamani ya Yen za Japan na shilingi ya Tanzania ikilinganishwa na dola ya Marekani*




Alisema kuwa Mradi huo, utaboresha usalama na ufanisi wa shughuli za upakiaji wa abiria na upakuaji wa mizigo kwa kukarabati jengo la abiria la Bandari ya Kigoma na ujenzi wa ghala la kuhifadhia mizigo litakalo gharamiwa na Serikali ya Tanzania na kujenga barabara unganishi za kuingia na kutoka bandarini ambako kutachangia kuimarika kwa biashara na usafirishaji katika maeneo husika.

Vilevile, Dkt. Mwamba alisema kuwa upatikanaji wa fedha hizo ni mwendelezo wa ufadhili kutoka Serikali ya Japan katika miradi ya maendeleo ambapo Tanzania inanufaika katika maeneo ya sekta za kilimo, maji, afya, nishati, usafirishaji, uendelezaji wa miji, elimu na usimamizi wa fedha za umma.

Aidha, Dkt. Mwamba aliihakikishia Serikali ya Japan utayari wa Tanzania chini ya uongozi wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuendelea kuimarisha ushirikiano kwa maendeleo ya wananchi wa pande zote na kwamba itachukua hatua zote muhimu kuhakikisha mradi huo unatekelezwa kikamilifu ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Kwa upande wake Balozi wa Japan nchini Tanzania, Mhe. Yasushi Misawa, alisema kuwa wametoa msaada wa fedha za mradi wa ukarabati wa Bandari ya Kigoma kwa kuwa utasaidia katika ukuaji wa uchumi na masuala ya kijamii.

Alisema kutokana na kushuka kwa kasi kwa viwango vya ubadilishaji fedha kwa miaka ya hivi karibuni na kupanda kwa gharama za bidhaa na mafuta kutokana na mgogoro wa Ukraine na Urusi, Serikali yake ilitambua kutakuwa na ukosefu wa fedha katika mipango iliyokuwa imewekwa awali ndio sababu ya kuongeza fedha za mradi huo.

# WATUMISHI WIZARA YA FEDHA WAHIMIZWA KUENDELEA KUCHAPA KAZI



*Na. Saidina Msangi na Farida Ramadhani*

Watumishi wa Wizara ya Fedha wameagizwa kuimarisha mfumo wa ukusanyaji wa mapato na kuratibu upatikanaji wa fedha ili kutoa fedha kwa wakati kwa ajili ya kutekeleza miradi yote iliyoidhinishwa na Bunge.

Wito huo ulitolewa na Naibu Waziri wa Fedha, Mhe. Hamad Hassan Chende (Mb), kwa niaba ya Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), wakati akifungua Kikao cha Watumishi na Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara kilichofanyika katika Ukumbi wa Mihadhara wa Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini (IRDP), jijini Dodoma.

Alisema kuwa ni muhimu watumishi hao kutekeleza majukumu yao na maelekezo yanayotolewa na Serikali kwa wakati ikiwa ni pamoja na kufanyia kazi kwa wakati yatokanayo na mjadala wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2024/25.

*"Ni muhimu kuwa mfano katika kuzingatia miongozo ya usimamizi wa mali na fedha za Umma, hususan katika kufungamanisha mahitaji yetu na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge pamoja na kuimarisha mfumo wa ushirikishaji, uratibu na kufanya kazi kwa karibu na wadau wetu ili kuongeza ubora wa huduma zetu kwa wateja wa ndani na nje", alisisitiza Mhe. Chande.*



Aliwaelekeza Watumishi hao kutumia taaluma zao katika kushauri na kufanya maamuzi kwa wakati kwa maslahi mapana ya Taifa pamoja na kufanyakazi kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Miongozo iliyopo ili kuimarisha mfumo wa utawala bora na utawala wa sheria.

Aidha, aliwaagiza Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo, kuendelea kusimamia majukumu waliyopewa katika Taasisi wanazoziongoza na kuongeza ubunifu na weledi ili kuweza kuchangia fedha katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

Alisema ni muhimu kusimamia majukumu yao kwa kuzingatia Sheria na Kanuni, mali na fedha za Serikali ikiwemo kudhibiti matumizi mabaya ya fedha za Umma katika ununuzi.

*Lengo la kujumuisha masuala ya maisha ya watumishi nje ya utumishi wa Umma ni kukumbushana kuwa sisi watumishi ni sehemu ya Umma, na pia inawezekana leo ni watumishi wa Umma lakini kesho tukawa raia kama raia wengine nje ya utumishi wa Umma"alieleza Bi Omolo.*

Akizungumzia utekelezaji wa majukumu ya Wizara, Naibu Katibu Mkuu, Bi. Jenifa Christian Omolo, alisema kuwa Wizara imeendelea kusimamia kwa ufanisi utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2023/24, bila kusahau changamoto mbalimbali zilizosababishwa na mabadiliko ya tabianchi.

Alisema wizara imeendelea kutoa huduma kwa wateja kwa mujibu wa Muundo na Mgawanyo wa Majukumu ya Serikali, kubuni na kusimamia utekelezaji wa Sera za Uchumi Jumla, Fedha na Ununuzi wa Umma pamoja na kusimamia ukusanyaji wa mapato na utaratibu wa upatikanaji wa fedha kutoka kwa wadau mbalimbali wa maendeleo.



*Tumeendelea kuratibu upatikanaji wa fedha na kuimarisha uhusiano wa masuala ya fedha kwa Taasisi za Kikanda na Kimataifa, kutekeleza maelekezo ya viongozi na kushiriki katika shughuli mbalimbali za pamoja za kitaifa ikiwemo michezo ya Mei Mosi, SHIMIWI, maonesho ya SABASABA, Nanenane n.k;", alifafanua Bi. Omolo.*





# BENKI YA DUNIA YAIMWAGIA SIFA TANZANIA UJENZI WA SGR

*Na Benny Mwaipaja*

BENKI ya Dunia imeipongeza Tanzania kwa hatua kubwa iliyopiga katika kutekeleza mradi wa kimkakati wa Reli ya Kisasa-SGR kwa kuwa ni miongoni mwa miradi itakayochochea ukuaji wa uchumi wa nchi pamoja na kuboresha huduma ya usafiri na usafirishaji kwa wananchi.

Pongezi hizo zilitolewa mjini Abuja nchini Nigeria na Makamu wa Rais wa Benki ya Dunia anayesimamia nchi za Ukanda wa Mashariki na Kusini mwa Afrika, Bi. Victoria Kwakwa, alipokutana na ujumbe wa Tanzania ukiongozwa na Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Kando ya Mikutano wa Mawaziri wa Fedha na Magavana wa Benki Kuu za Nchi za Afrika, ambazo ni wanachama wa Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa-IMF.

Bi. Kwakwa, alisema kuwa si rahisi kwa nchi nyingi za Afrika kujenga mradi mkubwa wa reli kama ilivyofanya Tanzania kwa kuwa ina gharama kubwa lakini kukamilika kwake kutachochea biashara katika eneo la Ukanda wa Maziwa Makuu huku akimmwagia sifa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuzindua rasmi safari za treni hiyo kutoka Dar es Salaam kwenda Dodoma.



Kwa Upande wao, Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba na Katibu Mkuu na Mlipaji Mkuu wa Serikali Dkt. Natu El-maamry Mwamba, walipokea pongezi hizo kwa niaba ya Serikali na kueleza kuwa lengo la mradi huo ni kuunganisha baadhi ya nchi za Ukanda wa Afrika Mashariki ili kufungua milango ya biashara.

Dkt. Nchemba alitumia mazungumzo hayo kuzitaka Taasisi za Fedha za Kimataifa ikiwemo Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa IMF, kuangalia uwezekano wa kuweka riba nafuu kwenye mikopo inayotolewa kupitia Madirisha ya Ujenzi wa Miundombinu ili nchi za Afrika ziweze kuboresha miundombinu ya usafiri na usafirishaji hatua itakayochangia kukamilisha miradi husika kwa wakati.

Benki ya Dunia ni mdau mkubwa wa maendeleo ya Tanzania ambapo imewekeza kiasi kikubwa cha fedha katika miradi mbalimbali ya kimkakati ya maendeleo pamoja na kuchangia Bajeti Kuu ya Serikali.



# TANZANIA KUJENGA KITUO CHA UMAHILI CHA HUDUMA YA MATIBABU



*Na Benny Mwaipaja*

Tanzania inatarajiwa kuwa miongoni mwa nchi tano za Afrika zitakazonufaika na ujenzi wa mradi mkubwa wa Hospitali itakayokuwa na viwango vya dunia vya utoaji huduma za matibabu (African Medical Center of Excellence (AMCE), kupitia mradi unaotekelezwa na African Export-Import Bank (Afreximbank) kwa kushirikiana na Hospitali ya Chuo Kikuu cha King, iliyoko London nchini Uingereza.

Hayo yalielezwa na Afisa Mtendaji Mkuu wa Kituo cha Umahili cha Kimatibabu, Abuja, Bw. Brian Deaver, wakati Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, alipoongoza ujumbe wa Tanzania kutembelea ujenzi wa mradi wa aina hiyo, nje kidogo ya mji wa Abuja, nchini Nigeria.

Bw. Deaver alieleza kuwa Hospitali hiyo itakayokuwa na uwezo wa kulaza wagonjwa 500 kwa wakati mmoja, itatumia teknolojia ya kisasa ambayo haijawahi kutumika katika Bara la Afrika kwa ajili ya kutibu magonjwa ya kansa ya damu na seli mundu (sickle cell).

Alifafanua kuwa Hospitali hiyo pamoja na hospitali nyingine zitakazojengwa nchini Ghana, Kenya na Tanzania, zitatoa huduma mtambuka ikiwemo uchunguzi, matibabu, tiba kwa njia ya nyuklia, upasuaji, huduma baada ya upasuaji na huduma nyingine zinazojulikana kitaalam kama *oncology, haematology* na magonjwa ya moyo.



*Tunapotekeleza mradi huu tunalenga kutoa huduma bora za afya, kutoa mafunzo kwa wataalam wa afya, kufanya utafiti, kutoa ajira, kudhibiti mahitaji ya matumizi ya fedha za kigeni hususan dola na kukuza utalii wa kimatibabu kwa nchi za Afrika" aliongeza Bw. Deaver*

Wakizungumza baada ya kutembelea mradi huo unaotarajiwa kugharimu zaidi ya dola za Marekani milioni 260, Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba na Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Dkt. Natu Elmaanry Mwamba, walisema kuwa mradi huo wa mfano si tu kwamba utasaidia huduma za kimatibabu kwa wananchi, bali pia itakuwa sehemu ya utalii wa kimatibabu kwa watu kutembelea na kupata huduma hizo kutoka nje ya Tanzania.

Kwa upande wake, Kaimu Balozi wa Tanzania nchini Nigeria, Bi. Judica Nagunwa, alisema kuwa jitihada zinazofanywa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika sekta ya uchumi na matibabu, umelenga kuimarisha afya za Watanzania na kwamba ubalozi wake utatumia kila fursa kuhakikisha kuwa mradi huo unatekelezwa kwa manufaa ya Watanzania.

Afreximbank ni Taasisi ya Fedha ya kimajumui ya kimataifa (Pan-African multilateral financial institution) yenye majukumu ya kutoa fedha na kuendeleza biashara kwenye nchi za Afrika.









# DKT. NCHEMBA AIHAKIKISHIA JUMUIYA YA KIMATAIFA KUBORESHA MIFUMO YA KODI

*Na Benny Mwaipaja*

Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), ameihakikishia Jumuiya ya Kimataifa na Watanzania kwa ujumla kwamba Serikali inaendelea kuweka na kuboresha mazingira ya uwekezaji ikiwemo kuboresha mifumo yake ya kodi.

Dkt. Nchemba aliyasema hayo katika Ofisi Ndogo za Wizara ya Fedha, Jijini Dar es Salaam, wakati akiagana na Balozi wa Uswisi aliyemaliza muda wake wa ubalozi hapa nchini, Mhe. Didier Chassot.

Alisema kuwa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ameunda Timu ya Wataalam ya kupitia na kuja na mapendekezo yatakayosaidia kuboresha mifumo yake ya kodi ili kuvutia zaidi biashara na uwekezaji nchini.

Mhe. Dkt. Nchemba, alifafanua kuwa pamoja na kuundwa kwa Timu hiyo, Serikali pia imechukua hatua kadhaa za kuboresha mifumo ya kielektroniki ya ukusanyaji kodi inayosaidia kukusanya mapato yake kwa ufanisi na kuondoa usumbufu kwa walipa kodi.

Alisema kuwa lengo la kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji pamoja na kuimarisha mifumo ya kodi ni kuhakikisha kuwa idadi ya walipakodi



inaongezeka hatua itakayosaidia pia kuiwezesha Serikali kupunguza viwango vya kodi ya ongezeko la thamani siku za usoni kwa sababu walipakodi watakuwa wengi.

Kwa upande wake Balozi wa Uswisi aliyemaliza muda wake hapa nchini, Mhe. Didier Chassot, aliipongeza Serikali kwa uamuzi huo wa kupitia mifumo ya kodi na kwamba anaamini Mabalozi wanaoziwakilisha nchi zao hapa nchini watapata pia nafasi ya kuzungumza na kujadiliana na Serikali kuhusu masuala hayo kama walivyoomba.

Mhe. Balozi Chassot, alitumia fursa hiyo ya kuagana na Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), kuipongeza Serikali ya Awamu ya Sita kwa hatua kubwa iliyopiga kimaendeleo katika kipindi kifupi.

Aliahidi kuwa Uswisi inaandaa mpango mpya wa ushirikiano wa kimaendeleo na Tanzania, utakaojielekeza katika kufanikisha agenda mbalimbali za maendeleo ya nchi kupitia program zake mbalimbali ikiwemo kusaidia mfuko wa maendeleo ya jamii-TASAF, usimamizi wa fedha za umma, biashara na uwekezaji kupitia asasi za kiraia na sekta binafsi.

Mhe. Didier Chassot, ameitumikia nafasi hiyo ya ubalozi akiwa hapa nchini kwa kipindi cha miaka minne na ameahidi kuendelea kuwa Balozi mzuri wa Tanzania atakaporejea nchini kwake kuendelea na majukumu yake mengine.

# MAMLAKA ZA SERIKALI NA SEKTA BINAFSI ZATAKIWA KUTUMIA FURSA ZILIZOPO KATIKA SHERIA YA PPP







*Na. Peter Haule na Joseph Mahumi*

Waziri wa Fedha Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb) ametoa rai kwa Mamlaka za Serikali pamoja na wawekezaji kutoka Sekta binafsi kutumia fursa zilizopo katika Sheria ya Ubia kati ya Sekta Binafsi na Sekta ya Umma (PPP) kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ili kupata faida na kuipunguzia Serikali mzigo wa kibajeti.

Mhe. Dkt. Nchemba alitoa rai hiyo Mjini Dodoma, wakati akifungua mafunzo ya kuwajengea uwezo Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi wa Halmashauri, Waganga Wakuu wa Mikoa na Waganga Wakuu wa Wilaya, kuhusu Sheria ya Ununuzi wa Umma, sura Na. 410, Sheria ya Ubia kati ya sekta ya Umma na Binafsi, Sura Na. 103 na mafunzo ya matumizi ya Takwimu zinazozalishwa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu, katika Ukumbi wa Mikutano wa Jiji la Dodoma, uliopo Mji wa Serikali Mtumba.

Aliwahimiza Maafisa Masuuli wote kuzingatia maelekezo ya Waraka wa Hazina namba 7 wa mwaka 2020/21 unaotoa maelekezo na mwongozo katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa utaratibu wa PPP.



Alisema kuwa Sheria ya PPP Sura 103 imefanyiwa marekebisho kwa kuweka mazingira wezeshi ili kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi katika kutekeleza miradi ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi, Sheria hiyo inaruhusu wawekezaji katika miradi ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi kunufaika na vivutio vya kikodi na visivyokuwa vya kikodi, sawa na wale wanaopata vivutio chini ya Sheria ya Uwekezaji Tanzania, Sura ya 38.

*Sheria ya PPP inaruhusu taasisi za umma kununua mbia anayekidhi vigezo moja kwa moja kwa miradi isiyohitaji ushindani ili kupunguza muda wa hatua za ununuzi na pia imetoa fursa kwa wawekezaji wa kigeni kushirikisha wazawa katika miradi ya PPP ili kuwawezesha kiuchumi na kuendeleza wataalamu wa ndani", alisema Dkt. Nchemba.*



Akizungumzia suala la matumizi sahihi ya Takwimu, Dkt. Nchemba alisema kuwa maendeleo ya Taifa lolote ulimwenguni yanatokana na matumizi sahihi ya takwimu zilizozalishwa na vyombo vyenye jukumu hilo katika kupanga mikakati mbalimbali ya maendeleo.

Alisema kuwa utekelezwaji wa mipango yote ya mendeleo nchini Tanzania umekuwa ukifanywa kwa kuzingatia takwimu zilizoandaliwa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu ambayo ilianzishwa kwa Sheria ya Takwimu ya Mwaka 2015 ambayo imeipa mamlaka ya kuandaa na kuchapisha takwimu mbalimbali zinazohitajika kwa matumizi ya kimaendeleo ikiwemo kiuchumi, kijamii na kisiasa.

Mhe. Dkt. Nchemba alisema pamoja na kuwepo kwa Ofisi ya Taifa ya Takwimu inayofanya kazi nzuri ya kutoa takwimu mbalimbali, bado matumizi ya takwimu hizo katika upangaji na utekelezaji wa mipango hauridhishi, kwa kuwa mara kadhaa imetiliwa mashaka kama ilitumia takwimu sahihi kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu.






Kwa upande wake Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mhe. Dkt. Festo Dugange, alisema kuwa katika historia ya nchi ya Tanzania hakuna kipindi ambacho Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mikoa zimetekeleza miradi mingi kama kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita.

Amesema bajeti kubwa ya Serikali inaenda TAMISEMI na kwa kiasi kikubwa inatumika kwenye ununuzi katika utekelezaji wa miradi lakini pia shughili mbalimbali za kiofisi.

Alisema kuwa katika taarifa nyingi za Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), kumekuwa na changamoto kubwa kwenye eneo la ununuzi, hivyo mafunzo hayo ni fursa muhimu kwa watendaji walioshiriki ili kuweza kutekeleza shughuli zao hususani za ununuzi lakini kutumia takwimu sahihi kupanga mipango ya maendeleo.

Akizungumza kwa niaba ya Wakuu wa Mikoa walioshiriki Mafunzo hayo, Mkuu wa Mkoa wa Geita, Bw. Martin Shigella, alisema kuwa wanapopata majukwaa ya mafunzo kama hayo yanasaidia kujua jambo gani la kufanya ili kusukuma jambo ambalo limekwama katika mkoa husika.

Aidha alimshukuru Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Nchemba kwa kuwaalika na wapo tayari kufanyia kazi yale yote yatakayowasilishwa kupitia mada mbalimbali katika kusukuma gurudumu la maendeleo.



# DKT. NCHEMBA ATOA WITO KWA NCHI ZA AFRIKA KUHIMIZA MATUMIZI YA NISHATI SAFI YA KUPIKIA



*Na. Benny Mwaipaja*

Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), ametoa wito kwa nchi za Afrika kutafuta njia na mikakati ya kuboresha uchumi na maisha ya wananchi wake kwa kutumia nishati safi ya kupikia ikiwa ni hatua pia ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya Tabianchi yanayochangiwa na uharibifu wa mazingira.

Dkt. Nchemba alitoa wito huo mjini Antananarivo nchini Madagascar kwa niaba ya Mhe. Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wakati akihutubia katika Mkutano wa Mwaka wa Wanahisa wa Taasisi ya Africa50 (General Shareholders Meeting - GSM) na Jukwaa la Miundombinu la Afrika (Infra for Africa Forum meeting) Taasisi ambayo Tanzania ni mwanachama, uliofanyika leo tarehe 19 Septemba, 2024, katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Ivato, na kufunguliwa na Rais wa Nchi hiyo, Mhe. Andry Rajoelina.

Aidha, Dkt. Nchemba alizishauri nchi hizo kuwekeza katika kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa wananchi wao kutumia nishati safi ya kupikia pamoja na faida zinazoambatana na utunzaji wa mazingira kiuchumi na kijamii.




Mkutano wa Wanahisa wa Africa50, uliwakutanisha wadau mbalimbali kutoka Bara la Afrika na duniani kwa ujumla wakiwemo Wawekezaji kutoka Taasisi za Umma na Sekta Binafsi, wakopeshaji, wataalam wa ujenzi wa miundombinu na kuwawezesha kutafuta suluhisho la changamoto za miundombinu katika Bara la Afrika pamoja na kukabikliana na athari za mabadiliko ya tabianchi na watahimizana kuhusu matumizi ya nishati safai ili kuchochea uchumi na maendeleo ya nchi hizo.

Dkt. Nchemba pia alitoa wito kwa taasisi za fedha na sekta binafsi kushiriki katika kampeni ya matumizi ya Nishati safi ya kupikia ikiwemo gesi iliyosindwa, Nishati ya jua, umeme wa joto ardhi, biogas, kwa kuwezesha upatikanaji wa fedha na pia kuzalisha vifaa ama majiko yanayotumia nishati hiyo.





# DKT. NCHEMBA APOKEA TAARIFA YA UTEKELEZAJI YA MWAKA YA PPRA








*Na Benny Mwaipaja*

Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Madelu (Mb), amepokea Taarifa ya Tathmini ya Utendaji Kazi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA), kwa mwaka wa fedha 2023/2024, katika Ofisi Ndogo za Wizara ya Fedha Jijini Dar es Salaam, 28 Septemba, 2024, na kuiagiza Menejimenti na Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka hiyo kuhakikisha kuwa watoa huduma wanaopata zabuni kupitia Mfumo wa Ununuzi wa Kieletroniki wa NeST, wanatumia malighafi na bidhaa zinazozalishwa ndani ya nchi isipokuwa kwa bidhaa ambazo ni lazima ziagizwe nje ya nchi kutokana na kutopatikana hapa nchini, hatua ambayo amesema itakuza uzalishaji wa bidhaa na huduma za ndani, kukuza ajira, kuongeza wigo wa kodi na kuchangia maendeleo ya nchi kupitia utekelezaji wa miradi mbalimbali inayotekelezwa na Serikali.

Aidha, Dkt. Nchemba amezitaka Taasisi za umma nchini kuhakikisha zinatumia Mfumo wa Ununuzi wa Umma wa Kielektroniki (NeST) kwakuwa hakuna mbadala wake ili kuongeza uwazi na uwajibikaji na udhibiti wa ndani wa Taasisi nunuzi, na hivyo kuendana na maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, aliyeitaka Wizara ya Fedha kudhibiti matumizi ya fedha za Serikali hasa kwenye utekelezaji wa miradi ili iendane na thamani ya fedha inayotumika kutekeleza miradi husika.

# WIZARA YA FEDHA YATOA MAFUNZO MFUMO WA UANDAAJI NA USIMAMIZI WA BAJETI (CBMS)





*Na. Peter Haule*

NAIBU Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Bi. Jenifa Christian Omolo, amefungua Kikao kazi cha mafunzo ya Mfumo wa Uandaaji na Usimamizi wa Bajeti (CBMS) ulioboreshwa ambacho kitaambatana na kufanya tathmini ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali ya Mwaka 2023/2024 ili kuweka mikakati itakayosaidia kuboresha uandaaji wa mipango na bajeti kwa mwaka 2025/2026.

Akizungumza jijini Dodoma kwa niaba ya Katibu Mkuu, Dkt. Natu El-maamry Mwamba, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Bi. Jenifa Christian Omolo, alisema kuwa lengo la kikao hicho lilikuwa kupata mafunzo ya Mfumo wa CBMS ulioboreshwa na kujadili kuhusu mafanikio na changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2023/2024 ili kubaini maeneo ya kuboresha.

Bi. Omolo alisema kuwa ushiriki wa wajumbe katika Kikao kazi hicho utasaidia kuboresha utekelezaji na usimamizi wa bajeti ya Serikali, kuongeza ufanisi katika mchakato wa bajeti na kuhakikisha vipaumbele vya Serikali vinatekelezwa ipasavyo.

Vilevile aliwataka washiriki wa kikao kazi hicho kushiriki kikamilifu katika mafunzo na kuuliza maswali yatakayowezesha kuuelewa vizuri na kuutumia Mfumo wa



vizuri na kuutumia Mfumo huo wa CBMS ili kuimarisha utekelezaji na usimamizi wa bajeti ya Serikali

Aidha, aliwafahamisha washiriki wa mafunzo kuwa mchakato wa maandalizi ya Mwongozo wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2025/2026 umeanza, hivyo ushauri na mapendekezo yatakayotokana na kikao kazi hicho yatasaidia katika kuboresha maandalizi ya Mwongozo huo.





Wizara ya Fedha katika kusimamia maadalizi na utekelezaji wa Bajeti ya Serikali, inafanya mafunzo ya Mfumo wa Uandaaji na Usimamizi wa Bajeti (CBMS) ulioboreshwa uliounganishwa na Mfumo wa Ulipaji Serikalini (MUSE) ili kurahisisha uingizaji wa takwimu za bajeti.





# Mimi tayari nime **Subscribe** unasubiri nini?




Muda ni Sasa! Pata taarifa, Makala na Vipindi mbalimbali kuhusu Wizara ya Fedha.

# KONA YA MAONESHO







KONA YA MAONESHO

# CAG KICHERE: BAJETI YA SERIKALI TOLEO LA MWANANCHI LAONGEZA UWAZI




Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Bw. Charles Kichere, ameipongeza Wizara ya Fedha kwa kuandaa yaliyomo kwenye Bajeti ya Serikali kwa lugha nyepesi (Toleo la Mwananchi) kwa kuwa inamsaidia mwananchi kuielewa bajeti ya nchi.

Bw. Kichere alitoa pongezi hizo alipotembelea Banda la Wizara ya Fedha wakati wa Maonesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa (Sabasaba) yaliyofanyika katika Viwanja vya Julius Nyerere Barabara ya Kilwa, Temeke, jijini Dar es Salaam.

Alisema kuwa kijitabu hicho ni sehemu ya uwazi na uwajibikaji kwa kuwa mwananchi wa kawaida anaweza kuelewa mipango ya Serikali katika kutekeleza maendeleo yao.





KONA YA MAONESHO

# NAIBU KATIBU MKUU, ELIJAH MWANDUMBYA ATEMBELEA BANDA LA WIZARA YA FEDHA SABASABA




Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Bw. Elijah Mwandumbya ametembelea Banda la Wizara ya Fedha katika Maonesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa (Sabasaba) yaliyofanyika katika Viwanja vya Julius Nyerere Barabara ya Kilwa, Temeke, jijini Dar es Salaam, ambapo alipongeza mikakati iliyowekwa ya kutoa elimu kwa umma kuhusu majukumu ya Wizara na Taasisi zake.

Bw. Mwandumbya alisema kuwa Wizara ya Fedha ni Wizara muhimu katika kuchochea maendeleo ya nchi hivyo ni muhimu elimu ikatolewa kwa usahihi na ufanisi ili Watanzania waweze kuelewa majukumu ya Wizara na Taasisi zake.

Alisema kuwa Maonesho hayo ambayo Idara, Vitengo na Taasisi za Wizara ya Fedha kwa pamoja zilitoa nafasi kwa watanzania kupata elimu kwa urahisi kuhusu Wizara hiyo.







KONA YA MAONESHO

# DKT. YONAZI AKOSHWA NA KOZI YA USALAMA WA MTANDAO VYUO VYA WIZARA YA FEDHA




Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu, Dkt. Jim Yonazi, amevipongeza Vyuo vilivyo chini ya Wizara ya Fedha kwa kuwa na programu zinazoendana na mabadiliko ya Sayansi na Teknolojia.

Dkt. Yonazi, alitoa pongezi hizo alipotembelea Banda la Wizara ya Fedha katıka Maonesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa (Sabasaba) yaliyofanyika katika Viwanja vya Julius Nyerere Barabara ya Kilwa, Temeke, jijini Dar es Salaam ambapo Vyuo hivyo kikiwemo Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM), kimeanzisha Kozi ya Usalama Mtandaoni (Cyber Security).






KONA YA
MAONESHO

# KAMISAA MAKINDA AWATAKA WANANCHI KUTUMIA TAKWIMU SAHIHI KWA MAENDELEO




Kamisaa wa Sensa na Spika Mstaafu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Anne Semamba Makinda, ametoa rai kwa wananchi kutumia takwimu sahihi zilizopatikana kutokana na Sensa iliyo fanyika katika shughuli mbalimbali za Maendeleo.



Mhe. Makinda alitoa rai hiyo alipotembelea Banda la Wizara ya Fedha katika Maonesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa (Sabasaba) yaliyofanyika katika Viwanja vya Julius Nyerere Barabara ya Kilwa, Temeke, jijini Dar es Salaam, ambapo alisisitiza matumizi ya Takwimu sahihi kwa maendeleo.



Alisema kuwa Takwimu zilizotokana na Sensa zina kila kitu hivyo ni vyema zikatumika kikamilifu katika mipango ya maendeleo lakini pia kutumiwa na watafiti wakiwemo wa vyuo mbalimbali katika kupata majibu ya changa-moto zinazoikabili jamii.





Mkurugenzi wa Idara ya Habari (Maelezo) na Msemaji Mkuu wa Serikali, Bw. Thobias Makoba (wapili kushoto), akisikiliza maelezo kutoka kwa Mchumi Mkuu Kutoka Idara ya Sera Wizara ya Fedha, Bi. Salome Kingdom (kulia), kuhusu umuhimu wa Sera ya Fedha katika maendeleo ya wananchi, wakati alipotembelea Banda la Wizara ya Fedha katika Maonesho ya Kimataifa ya Kilimo Nane Nane, yaliyofanyika Kitaifa katika Viwanja vya Nane Nane, Nzuguni, Jijini Dodoma.



Mkurugenzi Mkuu wa Kituo cha Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP Centre), Bw. David Kafulila (kushoto), akisikiliza kwa umakini maelezo ya Afisa Hesabu kutoka Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, Bi. Mercelina Haule (kulia), kuhusu, majukumu ya Huduma ya Mfuko Mkuu, alipotembelea Banda la Wizara ya Fedha katika Maonesho ya Kimataifa ya Kilimo Nane Nane, yaliyofanyika Kitaifa katika Viwanja vya Nane Nane, Nzuguni, Jijini Dodoma.



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Bi. Jenifa Christian Omolo (kulia), akisoma Kitabu cha Hali ya Uchumi Toleo la Mwananchi, wakati alipotembelea Banda la Wizara ya Fedha katika Maonesho ya Kimataifa ya Kilimo Nane Nane, yaliyofanyika Kitaifa katika Viwanja vya Nane Nane, Nzuguni, Jijini Dodoma.



Afisa Usimamizi wa Fedha Mwandamizi kutoka Idara ya Uendelezaji Sekta ya Fedha, Wizara ya Fedha, Bi. Mary Mihigo, akitoa elimu ya fedha kwa mmoja ya wananchi, Bw. Alhaji Hassan, alipotembelea Banda la Wizara ya Fedha katika Maonesho ya Kimataifa ya Kilimo Nane Nane, yaliyofanyika Kitaifa katika Viwanja vya Nane Nane, Nzuguni, Jijini Dodoma.

# KONA YA MAONESHO




Afisa Usimamizi wa Fedha, kutoka Idara ya Uchambuzi wa Sera, Wizara ya Fedha, Bw. Fronto Furaha, akiwaelezea wanafunzi wa Shule ya Msingi Bishop Stanway ya jijini Dodoma, majukumu ya Wizara ya Fedha katika kusimamia Uchumi, wakati walipotembelea Banda la Wizara ya Fedha, katika Maonesho ya Kimataifa ya Kilimo Nane Nane, yaliyofanyika katika viwanja vya Nane Nane, Nzuguni, Jijini Dodoma.




Katibu Mtendaji wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Bw. James Sando, akipata maelekezo kutoka kwa Mchumi Mwandamizi, kutoka Idara ya Usimamizi wa Madeni, Wizara ya Fedha, Bw. Sepo Seni, alipotembelea Banda la Wizara ya Fedha katika Maonesho ya Kimataifa ya Kilimo Nane Nane, yaliyofanyika Kimataifa katika viwanja vya Nane Nane, Nzuguni, Jijini Dodoma.



Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Bi Rosemary Senyamule, (wakwanza kulia), akitembelea Idara na Taasisi mbalimbali za Wizara ya Fedha, alipotembelea Banda la Wizara ya Fedha, katika Maonesho ya Kimataifa ya Kilimo NaneNane, yalinayofanyika Nzuguni, Jijini Dodoma.


















Matukio Mbalimbali ya Wananchi waliotembelea Banda la Wizara ya Fedha, katika Maonesho ya Kimataifa ya Kilimo Nane Nane, yaliyofanyika katika viwanja vya Nane Nane, Nzuguni, Jijini Dodoma.


#KaribuBandaLaWizaraYaFedha










#KaribuBandaLaWizaraYaFedha

## KONA YA MAONESHO

Wizara ya Fedha imeibuka Mshindi wa Pili wa Jumla kwa upande wa Wizara zilizoshiriki Maonesho ya 48 ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam yaliyoandaliwa na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE), yaliyofanyika katika Viwanja vya Mwalimu Nyerere, Kilwa Road, Jijini Dar es Salaam, mwaka 2024.












# Kamera Yetu




Baadhi ya wajasiriamali wa Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba mkoani Mtwara, wakipatiwa mafunzo ya elimu ya fedha na Wizara ya Fedha wakishirikiana na Taasisi za Fedha pamoja na OR TAMISEMI.





Afisa Ushirika kutoka Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC), Bw. Adolf Ndunguru, akigawa vipeperushi vyenye mada mbalimbali ikiwemo mikopo, akiba uwekezaji kwa baadhi ya wananchi wa Wilaya vya Mtama mkoani Lindi, waliojitokeza kupata elimu ya masuala ya fedha.

Mkazi wa Wilaya ya Ruangwa mkoani Lindi, Bw. Cosmas Rashid, akisoma kipeperushi chenye taarifa kuhusu mikopo wakati wa program  ya elimu ya fedha iliyotolewa na Wizara ya Fedha ambapo mada mbalimbali zilifundishwa ikiwemo kujiwekea akiba, mikopo na uwekezaji.



Afisa Usimamizi wa Fedha kutoka Wizara ya Fedha, Bw. Stanley Kibakaya akiwaelekeza wafanyabiashara wa Soko la Chifu Kingalu lililopo Mkoani Morogoro, jinsi ya kupakua filamu maalumu ya kutoa elimu ya fedha.




Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb) akipanda mti wakati wa halfa ya kuweka Jiwe la Msingi kwa awamu ya kwanza kati ya awamu tatu za ujenzi wa Kampasi ya Babati ya Chuo cha Uhasibu Arusha.



Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb) (kulia), akipiga ngoma, alipowasili wilayani Misungwi, mkoani Mwanza kwa ziara ya kikazi kukagua miradi ya maendeleo inayojengwa na Serikali mkoani humo.



Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha, Bi. Amina Khamis Shaaban, akifuatilia majadiliano wakati wa Kikao cha Kwanza cha Kamati ya Maandalizi ya Mkutano wa Nne wa Kimataifa wa Ugharamiaji kwa Maendeleo Endelevu (Fouth International Conference on Financing for Development - FfD4, kilichofanyika jijini Addis Ababa, Ethiopia.

## Tufuatilie katika **Mitandao yetu ya Kijamii**

- mofURT
- mofURT
- urtmof
- urtmof
- Wizara ya Fedha Tanzania
- HazinaTv


LIMETOLEWA NA
KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI
WIZARA YA FEDHA
MJI WA SERIKALI - MTUMBA
MTAA WA HAZINA
S.L.P 2802, 40468 DODOMA, TANZANIA
www.mof.go.tz